

**YESU KRISTO NAFSI YA MUNGU
MWENYEWWE ILIYOFUNIKWA KATIKA
MWILI WA KIBINADAMU**

Wakolosai 2:9 “Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili.

Sikiliza kile Nabii wa Mungu alivyosema juu ya hilo:

Ufunuo mkuu kuliko zote ni wa uungu, uungu wake mkuu Bwana wetu Yesu Kristo. Huwezi ukapata mahali pa kuanzia mpaka umeamini hilo, Tembea mbele.....Hivyo ndivyo Petro alivyosema, “Tubuni, na halafu muuone uungu (Matendo 2:38) mbatizwe kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako, na halafu sasa uko tayari kuingia katika Roho”. Kitu cha kwanza upaswacho kujua ni uungu wa Kristo. Mimi ni Alpha na Omega mimi ni kutoka A mpaka Z; hakuna mwingine zaidi ya mimi nilikuwepo tangu mwanzo; Nitakuwepo mwishoni mimi ni aliyekuwepo, aliyepo na atakayekuja, mwenyezi” (Ufunuo 1:8). Fikiria hilo. Hivyo ndivyo tarumbeta ilivyosema [1]

Ufunuo wangu kwa Roho Mtakatifu ni: Kristo na Roho Mtakatifu ni mtu huyohuyo, ila tu katika hali tofauti. Kwa hiyo hapa amesimama Kristo, mwanakondoo. Tunajua Yeye alikuwa mwanakondoo. Amesimama hapa akiwa na kitabu mkononi mwake (Ufunuo 5:6-10), na pale tunamuona mpanda farasi mweupe unaona? Kwa hiyo hakuwa ni Roho Mtakatifu (ufunuo 6:1-2).

Sasa, hiyo ni moja ya siri za siku za mwisho, Ni kwa namna gani Kristo awe nafsi tatu katika mmoja. Siyo watu watatu tofauti: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, wawe ni miungu mitatu kama watu wa utatu wanavyojaribu kutuambia kuwa ni hivyo. Huo ni udhihirisho wa mtu huyohuyo mmoja, au unaweza ukaita ni huduma za utendaji

tatu. Kama unazungumza na mhuduma, huwezi ukatumia ofisihivyo nitawaambia.....kwa sababu Kristo asingeweza kusema, “Nitaiomba ofisi yangu, na Atawatumia, ninyi ofisi nyingine”. Tunajua hilo lakini kama unataka uliweke vizuri: Ni huduma tatu za utendaji wa Mungu mmoja, na wala siyo miungu mitatu; Huduma tatu za utendaji wa Mungu mmoja unaona? Na sasa yawezekanaje Kristo awe nje kule na farasi mweupe akiwa anashinda na amesimama hapa na kitabu katika mkono wake? Siyo hivyo; siyo Kristo angalia sasa, Roho Mtakatifu na ufunuo na Kristo ni.....Roho Mtakatifu ni Kristo katika umbile lingine. Hiyo ni kweli [2]

Kama hapo mwanzo, Mungu alikaa mwenyewe, kwa sababu yeye ni mmoja (wapekee) wa milele, hata hakuwa Mungu. Mungu ni kiumbe cha kuabudiwa.

Na yule logosi, kama tunavyo 1 lile Neno lililotoka kwa Mungu, ambalo kila mmoja anajua ni Malaika wa Bwana (Kutoka 23:20-22), au Neno la Bwana, ambalo liliwaongoza Waisraeli katika jangwa lote: Malaika wa Agano, yule Logosi ambaye alitoka kwa Mungu (Kutoka 13:21-22). Na baada ya hapo yule Logosi alifanyika mwili na akakaa kati yetu. Sasa, tuko katika Yoh. Mt. 1:1-3. Hapo mwanzo kulikuwako Neno; naye Neno alikuwa kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu” Na sasa; kama alivyoyatoa maisha yake kwa ajili yetu, halafu tena Roho wake anakuja tena juu yetu. Yesu alisema, katika siku ile mtajua kuwa mimi ni ndani ya baba, na Baba ndani yangu, Nami ndani yenu, na ninyi ndani yangu” (Yohana 14:20).

Unaona, Ni Mungu wakati wote, Mungu akijidhihirisha mwenyewe, akitenda Yeye mwenyewe katika nyakati tofauti. Kwa hiyo hawa watatu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, Mungu yule yule akitenda katika hali tatu za udhihirisho.....Na sisi leo tu mmoja, kanisa lenyewe, likiwa ni udhihirisho wa mawazo ya Mungu. Kabla ya kuwekwa misingi ya dunia kulikuwa na kanisa kwa hiyo hao walio ndani ya Kristo walikuwa ndani ya Kristo hapo Mwanzo; ambao walikuwa ni mawazo yake, na mawazo yake katika udhihirisho wake [3]

Unaona Mungu alifanya vyote viwili yai na mbegu. Waprotestant kwa sehemu huamini kuwa ilikuwa ni Maria aliyetoa lile yai. Kama

hiyo ni hivyo, angalia kile unachomuwaia Mungu kufanya. Yai haliwezi kutolewa bila ya msisimko. Aliumba vyote viwili katika tumbo la Maria na mtu yule hakuwa chochote ila Mungu mwenyewe akifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, Emmanuel (Matayo 1:18-23). Siyo tu mtu mzuri tu, nabii; Alikuwa mtu mzuri na Nabii. Siyo mwalimu, mthiologia, oh, anaweza akawa hivyo vyote; alikuwa yote katika yote. Lakini juu ya yote, Alikuwa ni Mungu mwenyewe. Biblia ilisema tunaokolewa kwa Damu ya Mungu (Ufunuo 1:5-6 Matendo 20:28) Mungu mwenyewe, siyo nafsi ya tatu au nafsi ya pili, Ni ile nafsi, Mungu mwenyewe, Yehova mkuu akifunikwa ndani ya Mariamu katika uumbaji, na akaumba zile chembe zote mbili za damu (ule uhai) na hata yai pia [4]

Roho Mtakatifu alikuja juu yake (Yesu Kristo) pale mwanzoni mwa Yohana, naye akawa mesiya aliyepakwa mafuta sasa kumbuka, alipozaliwa alikuwa mwana wa Mungu. Alikuwa mwana wa Mungu aliyezaliwa kibikira. Lakini alipokuwa masihi, pale Roho Mtakatifu alipokuja juu yake, kwa sababu masihi maana yake ni “mpakwa mafuta”. Na YeYe alikuwa ni mpakwa mafuta pale Roho Mtakatifu alipokuja juu yake (Matayo 3:13-17) [5]

Mungu, ndani ya mtu, amejimwaga mwenyewe Yoeli 2:28, tunaona alisema, “Nitamwaga Roho wangu katika siku za mwisho” sasa kama utaliangalia lile Neno pale, Neno la Kigiriki.....Ninaweza nikakosea hapa, lakini lile moja nililolipata.....lazima uyaangalie maneno.

Kile kiingereza wakati mwingine kina maana mbili kama vile neno, tunasema ‘Mungu’ Mungu aliumba mbingu na nchi Mwanzo 1:1. Lakini sasa, katika Biblia ilisema, “Pale Mwanzo Elohim” sasa Elohim, kiingereza kinaita ² “Mungu” lakini haikuwa hasa Elohim chochote chaweza kuwa Munguhili neno “Mungu” unaweza kufanya sanamu Mungu; unaweza kufanya piano ni Mungu unaweza ukafanya chochote Mungu

Lakini sivyo ilivyo kwa neno “Elohim” Linamaanisha “Yule aishie Yeye mwenyewe” unaona? Lile piano haliwezi kuishi lenyewe; na hakuna chochote kiwezacho kuishi chenyewe kwa hiyo Neno

“Elohim” lamaanisha” Yeye ambaye siku zote aliishi” “Mungu” inaweza ikamaanisha chochote unaona tofauti katika neno?

Sasa, inaposema hapa alijimwaga mwenyewe au kujimwaga nje, tukafikiri kama hivi kwamba yeye “alitapika”, neno la kiingereza la kujimwaga au kujitoa nje kutoka kwake, kitu Fulani kilitoka kwake ambacho kilikuwa tofauti na YeYe” lakini neno”Kenos” kwa kigiriki halimaanishi kwamba “Alitapika nje” au kama- mkono wake ulitoka nje, au jicho lake lilitoka kuwa mtu mwingine,

Hilo linamaanisha, Alijigeuza mwenyewe; “akajimwaga mwenyewe ndani ya (Amen), ndani ya pazia (sura) nyingine katika hali nyingine; siyo nafsi nyingine ilitoka ndani yake iitwayo Roho Mtakatifu, lakini ilikuwa Yeye mwenyewe unalipata hilo? Yeye mwenyewe alijimwaga ndani ya watu Kristo ndani yako jinsi lilivyo la kupendeza, lilivyo la ajabu kufikiri, Mungu akijimwaga mwenyewe ndani ya wanadamu, ndani ya mwaminio; kujimwaga (Matendo 2:14-21) ilikuwa ni sehemu ya mchezo wa igizo kufanya hivyo Mungu, kwa utimilifu wote, uungu wote kwa jinsi ya mwili ulikuwa ndani ya mtu huyu Yesu Kristo (Kolosai 2:9) Alikuwa Mungu na Mungu pekee, siyo nafsi ya tatu au nafsi ya pili au nafsi ya kwanza; lakini ile Nafsi, Mungu akifunikwa katika pazia la ngozi ya kibinadamu.

1 Timothy 3:16; Bila shaka (kubishana) siri ya utauwa (uungu) ni kuu; Mungu Elohimu.....Herufi kubwa M-u-n-g-u katika Biblia ilionyesha kule mwanzo, yoyote yule, ilionyesha kule mwanzoni, ilisema, Elohim; kwa maana Elohim alifanyika mwili, na tukamshikashika Yeye” Elohim alifunikwa katika pazia la ngozi ya binadamu, Jehova mkuu aliyejaza anga yote (nafasi) muda, na kila mahali, alifanyika mtu. Tumemshikashika Yeye; Elohim “pale mwanzo Elohim.....Na Elohim akafanyika mwili, akakaa katika yetu (Yohana 1:14-18)”.

Angalia, utukufu wote ambao uko ndani ya Mungu uko ndani ya Neno. Baraka zote ambazo ziko ndani ya Mungu ziko kwenye Neno imefichwa kwa wasioamini na kanuni. Unaona ninachomaanisha? Lakini yote yako ndani ya Kristo. Vyote vile Mungu alivyo, alijimwaga mwenyewe (“Kenos”) na akaja ndani ya Kristo; na sisi, ndani ya Kristo tuko nyuma ya pazia.....

“Vema, Niko ndani ya Kristo unasema na tena unaamini kuna miungu mitatu? Unabatiza kwa jina la Baba na mwana na Roho Mtakatifu? Unaamini kanuni hizi zote unazoziamini na mambo haya unayoyaamini ya wazee? Hapana, bado uko nyuma ya pazia unaona? Njoo ndani ya pazia; Yeye Kristo ni Neno kwa vipi?

“Siamini juu ya uponyaji³ miungu, siamini juu ya miujiza hii na vitu kama hivyo”

Vema, unaona, huko ndani ya pazia; hujui chochote juu ya hilo unaona? Kristo ni Neno na tukiwa ndani ya Neno, tuko ndani ya Kristo. Na nawezaje kuwa ndani ya Kristo, huku ninamkataa Kristo? Ni yeye aliyesema, “Hapana neno moja litakaloongezwa au litakalopunguzwa (Ufunuo 2:18-19)” utawezaje sasa kupunguza na kuongeza hapo? Unaona, inaonyesha ni pazia gani ambalo limekufanya ufichwe mbali [6]

Yesu Kristo alikuwa ukamilifu wa Neno, kwa maana alikuwa utimilifu wa uungu kwa jinsi ya mwili, na ndani yake ulikaa utimilifu wa uungu. Mungu aliishi ndani ya Yesu Kristo. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake siyo myahudi au mmataifa, yeye ni Mungu (2Kor 5:19) pale amesimama, akijiumba mwenyewe jinsi linavyokubaliana..... na damu ya Mungu mwenyewe ilibidi imwagike chini, kutoka damu isiyo na hatia ya habili kuja chini, kutukomboa sisi. Hakuchukuwa maisha yake mwenyewe; hakuyazuilia maisha yake mwenyewe, Alisema, “baba, ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke mimi! Lakini, siyo nipendavyo, mimi mapenzi yako yatimie (Mt 26:36-42)” Alijitolea kwa lile Neno.

Leo tunaweza tukafanya jambo hilohilo unaweza uchukue kanuni zako, uchukue hii na hii, na uende popote pamoja nayo; lakini unaweza kusema, siyo nipendavyo mimi, lakini mapenzi yako yatimizwe” Njoo pale kwenye Neno la Mungu. Chukua mavazi ya urembo wako na Krismas na ufanye vyovyote upendavyo navyo, lakini nipe mimi Yesu Kristo moyoni mwangu. Haijalishi watu wangapi watacheka hilo, au vyovyote. Angalia tabia zake; uone

kama haifanyi kama alivyofanya kama haifanyi na hailingani na hili Neno iachilie mbali; siyo Kristo; kwa sababu Kristo ni Neno [7]

Na nisikieni mimi jambo baya sana lilikuwa gazetini siku ile nyingine kumruhusu mtu huyu mkuu, ambaye wote tunamjua kuwa ni mtumishi wa Mungu; Billy Graham. Alipoulizwa Billy Graham na watu fulani, Nini huu upinzani mkuu juu ya utatu? Je kulikuwa na Miungu mitatu, Miungu hasa mitatu au ikoje? Mmoja alionyesha kana kwamba ni miungu mitatu na mmoja ilionekana kwamba kulikuwa tu.....”Billy Graham alisema, “halijafunuliwa, hakuna ajuaye” jamani, kama kuna miungu mitatu, sisi ni wapagani.

Kama wayahudi walivyosema, “Ni yupi kati yao ni Mungu wenu ni Baba ni mwana ndiye Mungu wenu au ni Roho Mtakatifu ndiye Mungu wenu?” kuna Mungu mmoja tu na hawa siyo nafsi tatu, kwa sababu nafsi lazima iwe ni mtu haiwezi ikawa nafsi bila kuwa ni mtu, unajua hilo kitu chawaje ni nafsi bila ya kuwa ni mtu?

Oh, alisema, “hatuamini katika nafsi tatu binafsi za Mungu; tunaamini katika nafsi za Mungu yule yule mmoja” vema, kabla haijawa nafsi lazima iwe ni mtu.

Ni nini sasa? Utasema siyo mi⁴ mitatu ni ofisi tatu za Mungu yule yule. Alikuwa ni Baba pale mwanzoni aliyening’inia juu mawinguni kule jangwani katika mwali wa moto, moto uliowaka kwenye kijiti.....ule⁵ Mungu, nimemaliza tu kusema kule kujishusha, kuja chini; hiyo ule utaratibu mkuu. Roho, Agape, Zoe, ule uhai wa Mungu mwenyewe ukiwa katika namna ya nguzo ya moto.

Na huyu huyu mmoja baada ya kuwa katika ubaba, alikuwa mwana na ile Roho iliyokuwa katika kijiti kiwakacho moto ilikuwa ndani ya mtu Kristo na ilileta ushahidi uleule ambao ule moto ulileta. Alisema, “Kama sifanyi kazi za Baba yangu, msiniamini mimi (Yohana 14:10-12). Kila mti utaweka rikodi yake ya matunda uzaayo.

Unaona, ilishuka chini kutoka kiumbe cha kimiujiza kisichooneka kuja kwa kitu kinachoweza kushikika kile uwezacho kukishika, mwili (filipi 2: 5-11) Na kupitia kifo chakujitoa sadaka na dhabihu

iliyo kuu ya huyu Mungu mmoja Yesu, Alisema, “Mimi na Baba yangu tu mmoja. Baba yangu ankaa ndani yangu” unaweza.....Hakuna awezaye kusoma hilo kwa wazi zaidi. Walisema kwa nini hutuonyeshi sisi huyo Baba, na itatutosha sisi” Yohana 14:7-10.

Alisema, nimekuwa pamoja nanyi kwa muda mrefu nanyi hamnijui mimi? Alisema, “Unapomuona Baba.....ukiniona mimi umemuona Baba yangu” kama mwanamke mmoja aliruka juu nakusema, “kwa nini Ndg Branham,” alisema, Baba na Mwana ni mmoja, kama tu vile wewe na mke wako mlivyo mmoja”.

Nikasema, “oh hapana na siyo hawako hivyo” Nikasema “unaniona mimi? “akasema, “ndiyo” nikasema, unamuona mke wangu? “akasema, “hapana”

Nikasema, hawako sawa katika aina ya mmoja. Yesu alisema, “ukiniona mimi, umemuona Baba. Baba, ankaa ndani yangu. “Mke wangu hakai ndani yangu” unaona? Wao ni mmoja; katika kila namna ni mmoja. Na sisi tu mmoja kupitia makubaliano, mke wangu na mimi tuko mmoja katika ushirika, lakini sisi ni nafsi mbili. Mke wangu anaweza akafikiria kwa aina fulani na mimi kwa namna nyingine na sisi ni nafsi mbili lakini siyo hivyo kwa Mungu, Mungu na Kristo ni mtu huyohuyo mmoja.

“Sasa Roho Mtakatifu ni nini?” Roho mtakatifu ni Roho yuleyule wa Mungu akikaa ndani ya watu, ambao amewafia na kuweka majina yao katika kitabu cha uzima, ambao walikuwa mmoja pamoja naye hapo mwanzo maandiko yalisema hivyo. Je Yesu hakuwaambia kuwa alikuwa pamoja nao kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu? (Yohana 17:6-8-14-15)? Akili zenu zimetiwa giza na kivuli, sisi sote tuko hivyo kwa mambo hayo lakini sio tuko hapa kwa katukio kadogo kabahati; Tu wana na binti wa Mungu tangu mwanzoni mwa uumbaji wa Mungu (Ayubu 38:1-7). Na tumeshushwa hapa kuwa mashahidi wa kushuhudia

Neema za Mungu ambazomwagwa mioyoni mwetu na Roho Mtakatifu (Rumi 5:5) Tu.....Roho milele na hakuna namna ya

kulisimamisha hilo (kulizuia) kanisa la Mungu litakuwa pale kwa hakika kama uhakika uwezavyo kuwa [8]

Imani ni nini? Imani ni kitu fulani kinachofunuliwa kwako, ambacho bado hakijawa, lakini unaamini litakuwa. Imani ni ufunuo wa mapenzi ya Mungu kwa hiyo kwa ufunuo.....

Na makanisa leo hata hayaamini katika ufunuo wa kiroho. Waamini katika mafundisho ya kanuni za utaratibu fulani “kwa ufunuo Habili alitoa dhabihu iliyobora kwa Mungu kuliko ile ya kaini, ambaye Mungu alimshuhudia kuwa mwenye haki (Waebra 11:4)” Amen natumaini unaliona hilo unaona mahali tunapoishi, na saa yake?

Nilikuwa nazungumza na Muungwana mmoja sio muda mrefu uliopita, msomi wa Kikristo na muungwana. Alisema, “Bwana Branham, nakataa mafunuo yote”

Nikasema, “kwa hiyo unapaswa kumkataa Yesu Kristo, kwa maana yeye ni ufunuo wa Mungu, Mungu amefunuliwa katika mwili wa kibinadamu na mpaka umeliona hilo, sivyo umepotea.

Yesu alisema,”msipoamini kwamba mimi Ndiye, mtakufa katika dhambi zenu (Yohana 8:21-29)”

Yeye ni ufunuo wa Mungu, Roho wa Mungu akifunuliwa katika umbile la kibinadamu. Kama huwezi kuamini hilo,umepotea. Kama unamfanya Yeye nafsi ya tatu, nafsi ya pili au nafsi nyingine tofauti na Mungu, umepotea. Msiposadiki kwamba mimi ndiye mtakufa katika dhambi zenu” ufunuo sio ajabu hawakuweza kumuona yeye hakuna mtu awezaye kuja kwangu asipovutwa na Baba yangu (Yohana 6:44) na wote Baba alionipa (kule mizizini) watakuja kwangu (Yohana 6:37-39)” unaona? Unalipata hilo? Oh, jinsi tunavyopaswa kumpenda yeye, kumwabudu Yeye, kumsifu Yeye, kuona matunda ya Roho Mtakatifu yakiiva katika mti wa Bibi arusi juu ya wakati [9]

Sasa, ili kujifunza maandikoPaulo alimwambia Timothy (2Tim 2:15), “jifunze hayo ukiligawanya kwa usahihi Neno la Mungu ambalo ni kweli” Sasa kuna mambo ya lazima hufanya katika maandiko unapolitumia Neno la Mungu kuna mambo matatu

ambayo hupaswi kutenda. Sasa hebu tujifunze hayo kwa dakika kumi zijazo mambo matatu ambayo hupaswi kufanya.....na ninyi wote katika sehemu mbalimbali katika taifa lote, kuwa na uhakika kuyaweka haya mambo ndani ya nia yako, kuwa na uhakika kuyaweka haya mambo ndani ya nia yako kama hunapenseli. Hupaswi kufanya mambo haya tunawaambia wakati wote yale yawapasayo kufanya; sasa ninaenda kukuambia yale ambayo hupaswi kufanya.

Hupaswi kulitafsiri vibaya N----- Unasema “vema, naamini linamaanisha hivi” Linamaanii⁷ kile linachosema halihitaji mtafsiri. Na hupaswi kuliweka Neno mahali ambapo sipo pake. Na hupaswi kulitegua Neno na kama tutafanya mojawapo ya hayo, inaitupa Biblia katika machafuko na vurugu.

Angalia kumtafsiri vibaya Yesu ni umbo la Mungu katika mwili wa binadamu utamfanya yeye Mungu mmoja kati ya watatu kumtafsiri vibaya Yesu Kristo yeye akiwa Neno, utamfanya yeye Mungu mmoja kati ya watatu, au utamfanya yeye kuwa nafsi ya katika uungu. Na kufanya hivyo, utavuruga maandiko yote hutaweza kufika popote kwa hiyo halipaswi kutafsiriwa . Na kama unasema kwamba kitu fulani, unaweka tafsiri juu ya hilo, na unaliweka kwa wakati mwingine, bado unaweka tafsiri ambayo siyo sawa.

Kama mtu yoyote akimtafsiri vibaya Yesu Kristo katika Biblia kuwa Yeye siyo Mungu mwenyewe, kumfanya nafsi ya pili au Mungu mmoja kati ya watatu, hilo litavuruga kila Neno katika Biblia yote litavunja amri ya kwanza, “usiwe na miungu mingine ila mimi (Mwanzo 20:3)”. Vema itaifanya jamii yote ya wakristo kuwa kundi la waabudu wapagani waabuduo miungu mitatu tofauti. Unaona ni aina gani ya Biblia utakuwa nayo? Hilo litatufanya tuwe vile wayahudi wanavyotusema waliuliza. Ni yupi kati ya hao miungu ni Mungu wenu?” unaona? Kwa hiyo unaona, hupaswi kamwe hutafsiri vibaya Biblia, kwa kuwa Yesu mwenyewe ni tafsiri ya Biblia, anapodhihirishwa katika wakati, kwamba sehemu ya mwili wake inapodhihirishwa. Kama ni wakati wa mkono, lazima iweni mkono; haiwezi kuwa wakati wa kichwa kama ni wakati wa sauti, vema sasa, haiwezi kuwa wakati wa mguu. Unaona? Na sasa, tuko wakati wa macho. Na sasa, kinachofuatia ni Yeye mwenyewe kuja [10]

Unaona, siku zote nimehubiri kwamba Yeye ni Mungu, wala siyo mtu tu; Alikuwa Mungu akidhihirishwa katika mwili, Mungu, sehemu ya upendo wa Mungu, ile sehemu kubwa ya Mungu ambayo ilikuja chini ikadhihirishwa hapa duniani Yesu alikuwa Upendo wa Mungu, ambao ulijenga mwili wa Jehova mwenyewe alimoishi ndani. Alikuwa utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili. Vile Mungu alivyo. Alijidhihirisha kupitia ule mwili. Ule mwili ulipaswa ufe ili aweze kumwosha Bibi Arusi na Damu yake. Na angalia, siyo tu Bibi Arusi ameoshwa, na kusamehewa lakini amehesabiwa haki mbele za Mungu [11]

Nukuu za kiingereza

8

- (1) Maono ya patmo uk 97 Aya 1-3
- (2) Ule muhuri wa kwanza Aya 156 – 4/5 (268/269)
- (3) Ile mbegu haitarithi pamoja na kapi Aya 32
- (4) Ile mbegu haitarithi pamoja na kapi, Aya 100
- (5) Kumiliki malango ya Adui uk 16 Aya 79
- (6) Kufunuliwa kwa Mungu Aya 74-79,238
- (7) kwa nini bethlehemu mdogo Aya 129
- (8) Ubatizo wa Roho Mtakatifu Aya 90-97
- (9) Wapakwa mafuta wa siku za mwisho aya 53-56
- (10) Kristo anafunuliwa katika Neno lake Aya 72-76
- (11) Kunyakuliwa Aya 160 – 161

jiwe la kiroho la kujengea na 161 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany Phone (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306.

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa: Charles E. Y. Kanju, Box 5138, Tanga

E-mail: chaelika@hotmail.com

Cell.phone 0784704299